



**BENKI KUU YATOA KOMPYUTA MPAKATO KWA WANAFUNZI WA VYUO VIKUU  
INAOWASOMESHA**



*Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Dkt. Yamungu Kayandabila, akimkabidhi, Bw. Filimon Mugandu kompyuta mpakato yake na picha ya kulia wanufaika hao wa udhamini wa elimu katika picha ya pamoja na Msimamizi wa Mfuko huo, Bi. Consolata Shayo (wa pili kutoka kushoto).*

Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Dkt. Yamungu Kayandabila, amewataka wanafunzi wanaonufaika na Mfuko wa Udhamini wa Kumbukumbu ya Mwalimu Julius K. Nyerere unaondeshwa na Benki Kuu ya Tanzania kuhakikisha wanafanya vizuri katika masomo yao.

Ametoa wito huo, jana jioni Benki Kuu makao jijini Dar es Salaam wakati alipokabidhi kompyuta mpakato (laptops) kwa wanufaika sita wa Mfuko huo kwa mwaka wa elimu wa 2017/18 wanaosoma shahada za kwanza na za uzamili katika vyuo vikuu hapa nchini. Kompyuta hizo ni sehemu ya vitendea kazi vitakavyowasaidia katika masomo.

“Ninawashauri kuendelea kuzingatia masomo na kuwa wanafunzi wenye nidhamu. Mkifanya hivyo, mtakuwa mabalozi wema wa Mfuko wa Udhamini wa Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Nyerere...na mtaongeza idadi ya wataalam kama ilivyokuwa nia ya Mwalimu Nyerere kuwekeza katika elimu ili kupata wataalam wengi,” alisema Dkt. Kayandabila ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mfuko huo.

Mfuko huo ulianzishwa na Benki Kuu ya Tanzania mwaka 2009 kwa lengo la kuongeza hamasa na ufaulu wa masomo ya hisabati na sayansi miongoni mwa wanafunzi wa kike hapa

Tanzania. Aidha, udhamini huo pia hutolewa kwa wanafunzi wa kike na wa kiume kusoma masomo ya uchumi, teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), Uhasibu na Fedha kwa shahada ya kwanza na shahada ya uzamili.

Waliokabidhiwa kompyuta mpakato hizo ni wanafunzi wa shahada ya udaktari (medicine) katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Afya cha Muhimbili (MUHAS), Bi. Sophia Juma na Bi. Agatha Ninga na Bw. Rajab Mabaranga ambaye anasoma shahada ya kwanza ya Biashara (Fedha) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Wengine ni Bi. Ummul-Khair Mustafa anayesoma shahada ya Uzamili ya *Parasitology and Medical Entomology* MUHAS na Bw. Filimon Mugandu anayesoma shahada ya Uzamili ya hisabati (*Mathematical Modelling*) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Bi. Byera Kabairuka ambaye pia anasoma Shahada ya Udaktari MUHAS, hakuweza kuhudhuria hafla ya kukabidhiwa kompyuta mpakato.

**Wanufaika hao wa udhamini walichaguliwa kutoka miongoni mwa wanafunzi 10 bora kwa ufaulu katika mitihani ya taifa ya Kidato cha Sita kwa wanaosoma shahada ya kwanza na ufaulu mzuri wa shahada za kwanza kwa wanaosoma kozi za shahada ya uzamili.**

Wanafunzi hao sita waliodhaminiwa na Mfuko kwa mwaka 2017/18, wanafanya **idadi ya wanafunzi wote ambao wamepata udhamini wa Mfuko huo hadi hivi sasa kufikia 34. Kati yao, 12 wamekwishamaliza masomo yao ya shahada za kwanza na za uzamili na kupata ufaulu mzuri sana wa Daraja la Kwanza au Daraja la Pili la Juu katika masomo yao.**

Kwa upande wao, wanafunzi hao waliishukuru Benki Kuu ya Tanzania kwa kuanzisha Mfuko wa Udhamini wa Elimu wa Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Nyerere na kuahidi kwamba watafanya bidii katika masomo yao ili malengo ya kuanzishwa kwa mfuko huo yaweze kutimia.

“Tuna mambo mawili ya kufanya. Kwanza, ni kuonyesha kwamba tulistahili kupata udhamini huu wa masomo kwa kufaulu vizuri katika masomo yetu; na pili ni kuanza kufikiria namna ya kuirudishia jamii matunda ya elimu na ujuzi wetu. Elimu kama haisaidii kutatua matatizo katika jamii ni bure,” alisema Bw. Mugandu.



*Wanufaika wa udhamini wa elimu unaotolewa na Mfuko wa Udhamini wa Kumbukumbu ya Mwalimu Julius K. Nyerere wakati wa hafla ya kukabidhiwa kompyuta mpakato Benki Kuu jijini Dar es Salaam. Kutoka kulia ni Bi. Agatha Ninga, Bi. Sophia Juma, Bi. Ummul-Khair Mustafa, Bw. Rajab Mabaranga na Bw. Filimon Mugandu.*



*Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Dkt. Yamungu Kayandabila, akisikiliza maelezo kutoka kwa Msimamizi wa Mfuko huo, Bi. Consolata Shayo (katika picha inayofuata) huku baadhi ya wanafunzi na wajumbe wa Kamati ya Uchamini ya Mfuko huo wakifuatilia.*







***Kushoto:** Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Dkt. Yamungu Kayandabila (aliyekaa), katika picha ya pamoja na wanafunzi walionufaika na udhamini wa elimu ya juu; na **kulia** ni Naibu Gavana, wanafunzi na Wajumbe wa Kamati ya Udhamini ya Mfuko huo mwishoni mwa hafla ya kukabidhiwa kompyuta mpakato.*

Imetolewa na Idara ya Uhusiano wa Umma na Itifaki  
[botcommunications@bot.go.tz](mailto:botcommunications@bot.go.tz)  
Aprili 4, 2018